

**TAARIFA YA UDARAJISHAJI WA MAKAMPUNI YA WAENDESHA GHALA
KATIKA MSIMU WA UFUTA KWA MWAKA 2024/25**

Rejea somo tajwa hapo juu.

2. Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339 R.E 2016 **Kifungu cha 6(1) (a)** kinaipa WRRB mamlaka ya kufanya ukaguzi wa shughuli za upokeaji, uhifadhi na utunzaji wa bidhaa sambamba na ukaguzi wa ghala, bidhaa zilizohifadhiwa pamoja na ukaguzi wa nyaraka na kumbukumbu zinazohusika. Aidha, Bodi inayo mamlaka pia kisheria kupitia kumbukumbu na kufanya tathmini ya utendaji wa makampuni husika baada ya msimu.

3. Bodi imechakata utendaji wa makampuni mbalimbali yaliyopatiwa leseni kwa zao la ufuta kwa Msimu wa 2024/2025. Hadi tarehe 02 Agosti 2024 saa 4:00 asubuhi, jumla ya **leseni 48** zilitolewa kwa **Kampuni 34** za Waendesha ghala katika Mikoa ya Songwe, Ruvuma, Pwani, Lindi, Mtwara na Morogoro. Aidha, hadi muda huo, Kiasi cha ufuta uliopokelewa ni jumla ya **gunia 2,849,927.00 zenye uzito wa kilo 141,234,966.40.**

3. Baada ya kutolewa kwa leseni hizo kwa zao la ufuta kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za ghala, Bodi imefanya tathmini kwa kila kampuni iliyoshiriki kwenye msimu wa ufuta katika maeneo yafuatayo:

- i. Ukamilishaji wa maombi ya leseni ya Bodi pamoja na nyaraka zilizowasilishwa;
- ii. Uendeshaji wa shughuli za ghala katika msimu wa ufuta kwenye maeneo ya upokeaji mzigo, upangaji wa mzigo ghalani, utoaji wa mzigo na ukamilishaji wa nyaraka zinazotakiwa; na
- iii. Makosa mbalimbali yaliyofanywa na makampuni wakati wa utekelezaji wa kazi zake kwenye msimu wa huu ufuta kwa mwaka huu.

4. Kufuatia tathmini kwa kuzingatia vigezo vilivyo tajwa hapo juu, matokea yamegawanyika katika maeneo matatu kama ifuatavyo:

- i. Makampuni ambayo yanaweza kuendelea kufanya shughuli za Mfumo kwa kujisimimia zenyewe;
- ii. Makampuni ambayo kwa kuzingatia tathmini iliyofanywa hayawezi kufanya kazi yenyewe na hivyo kutakiwa kufanya yafuatayo;

- a) Kuwa chini ya usimamizi wa Bodi kwa gharama za kampuni ambazo zitalipwa katika vipindi vya wiki mbili mbili . Aidha, leseni itatolewa na ghala kufunguliwa baada ya taratibu hizo kukamilika.
 - b) Kutoa taarifa ya utendaji kila baada ya wiki mbili wakati wa utekelezaji wa shughuli za mfumo wa Stakabadhi ghalani.
- iii. Makampuni ambayo kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa, hayawezi kukidhi masharti ya leseni za Bodi na hivyo kuondolewa kwenye tasnia ya usimamizi wa Stakabadhi za ghala.

Matokeo ya tathmini husika ni kama inavyoonekana kwenye kimabatisho Na. 1 cha waraka huu.

Jedwali Na.1: Udarajishaji wa awali wa makapuni ya Waendesha ghala wa Ufuta		
Makampuni yanayoendelea	Makampuni chini ya uangalizi wa Bodi	Makampuni yatakayokosa sifa za kutekeleza Mfumo
1. Pugna Agrifood Tanzania Ltd 2. Nachingwea Investment And Supplies Ltd 3. Ahn & Raka Company Ltd 4. Inoliva Company Ltd 5. Sumajkt Logistic Company Limited 6. Pisah Limited 7. Dreams On Development Company Limited 8. Zuboma General Supplies 9. Demuton Tanzania Ltd 10.Makita Agrifood Limited 11.Ruangwa Warehousing Company Ltd 12.Saesh Business Company Limited 13.Bojomosa Agriventure Company Limited 14.Liwale Tabasamu Company Limited	1. Perfect Cashew Kernel Ltd 2. Kiibale Company Ltd 3. Mandiwa Agro Products Limited 4. Tanyusa Company Ltd 5. Khamoz Trading Co. Ltd	1. Ngonde Traders Company Limited Bin Swalehe General Dealers Ltd 2. Foremax Tanzania Limited 3. Geju Investment And General Supply Company Limited 4. Nampachila Business Company Limited 5. Synar Enterprises Company 6. Lenzaq Holdings Limited 7. Mkwajuni Trading Company Limited

15.Krenk Agro (T) Ltd 16.Zuma General Trading Company Limited 17.H & E Moonrich Comapny Limited 18.Ifwani General Supplies Co. Ltd 19.Mkaba General Traders Co.Limited 20.Rwk International (T) Limited 21.The Prominence Global Traders And Co Ltd		
---	--	--

Ifahamike kwamba, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Makampuni yaliyokosa sifa hawataruhusiwa kuhusika wala kufanya kazi kwenye Mfumo wa Stakabadhi za ghala.